MWONGOZO MFUPI WA SHERIA KWA MSAIDIZI WA KISHERIA

SHERIA ZA UKATILI DHIDI YA WANAWAKE NA WATOTO NCHINI TANZANIA

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KATIBA NA SHERIA

german cooperation
DEUTSCHE ZUSAMMENARBEIT

Implemented by:
giz Deutsche Gesellschaft für Internationale Zusammenarbeit (GIZ) GmbH

Published by

Deutsche Gesellschaft für Internationale Zusammenarbeit (GIZ) GmbH

Registered offices
Bonn and Eschborn, Germany

'Access to Justice for Women and Children / Society in Action for Equality' (SAFE)

GIZ Office Tanzania,
65, Ali Hassan Mwinyi Road,
Dar es Salaam, Tanzania
Tel: +255 22 211 5901
giz-tanzania@giz.de
safeproject@giz.de
www.giz.de

As at **August 2025**

Design **Trevor Livingstone**

Text **Lulu Urrio and Glory Sandewa**

GIZ is responsible for the content of this publication

On behalf of **Federal Ministry for Economic Cooperation and Development (BMZ)**

In cooperation with **Ministry of Constitutional and Legal Affairs (MOCLA)**

01

UTANGULIZI

UTANGULIZI

Serikali ya Tanzania imesaini na kuridhia mikataba yote mikuu ya kimataifa na kikanda ya kulinda na kutetea haki dhidi ya ukatili kwa wanawake na watoto. Mikataba hii imeingizwa kwa kiasi katika sheria mbalimbali za nchi kama vile Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (kama ilivyorekebishwa mara kwa mara), Sheria ya Kanuni za Adhabu Sura ya 16 (Mapitio ya 2022), Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329 (Mapitio ya 2022), Sheria ya Makosa ya Kimtandao ya mwaka 2015, na nyinginezo. Pamoja na kuanzishwa kwa mifumo inayojumuisha wadau mbalimbali ya ulinzi na usalama wa wanawake na watoto kuanzia ngazi ya kijiji/mtaa hadi taifa, kwa mujibu wa Mpango wa Kitaifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto.

Serikali ya Tanzania imesaini na kuridhia mikataba yote mikuu ya kimataifa na kikanda ya kulinda na kutetea haki dhidi ya ukatili kwa wanawake na watoto.

Hata hivyo, ukatili dhidi ya wanawake na watoto bado ni changamoto kubwa nchini Tanzania. Kwa mujibu wa Utafiti wa Afya na Idadi ya Watu Tanzania, asilimia 27 ya wanawake wa Kitanzania wenye umri kati ya miaka 15–49 wamewahi kufanyiwa ukatili wa kimwili, na asilimia 12 ukatili wa kingono. Zaidi ya hayo, asilimia 39 ya wanawake wa kundi hili wamefanyiwa ukatili wa kimwili au kingono kutoka kwa wenza wao. Ukatili uko zaidi vijijini (asilimia 41) kuliko mijini (asilimia 35).

Ukatili Dhidi ya Wanawake Tanzania – Takwimu Muhimu (TDHS)

27%
ya wanawake (umri 15–49) wamewahi kufanyiwa ukatili wa kimwili

12%
ya wanawake (umri 15–49) wamekumbwa na ukatili wa kingono

Ukatili ni mkubwa zaidi vijijini **(41%)**
ikilinganishwa na mijini **(35%)**

Ukatili dhidi ya wanawake na watoto ni sehemu kubwa ya ukatili wa kijinsia, unaotokana na ukosefu wa usawa wa kijinsia, nguvu zisizo sawa, na mila potofu. Wanawake na watoto mara nyingi huwa waathirika wakuu waukatili, wakikumbana na aina nyingi za ukatili kama vile ukatili wa nyumbani, ubakaji, na ukatili wa kihisia. Pia, jamii hujihusisha na kukubali ukatili kama njia ya kutatua migogoro au kudhibiti uhusiano, jambo linalochangia ukimya kutokana na unyanyapaa. Pamoja na changamoto za kisheria na za kitaasisi kwenye mahakama na vyombo ya maamuzi zenye huzuia upatikanaji wa haki kwa wahanga wa ukatili. Pia uwepo kwa uelewa mdogo wa sheria, ukosefu wa msaada wa kisheria, umbali na urasimu wa vyombo vya kisheria, pamoja na ucheleweshaji wa kesi unaosababisha wahalifu wa ukatili wa wanawake na watoto kutowajibika.

Wanawake na watoto mara nyingi huwa waathirika wakuu waukatili, wakikumbana na aina nyingi za ukatili kama vile ukatili wa nyumbani, ubakaji, na ukatili wa kihisia.

Wasaidizi wa kisheria wana mchango mkubwa katika kusaidia wahanga wa ukatili ndani ya jamii. Wanatambua mila na desturi za jamii zao, hivyo huweza kutoa ushauri wa kisheria unaolingana na muktadha, kusuluhisha migogoro, na/au kuwaunganisha wahanga na wataalamu wa sheria au watoa huduma wengine kama madaktari, polisi, maafisa ustawi wa jamii, huduma za kijamii na usaidizi wa kisaikolojia. Pia hutoa elimu na ushauri wa kisheria, taratibu za kisheria na ukatili wa kijinsia kwa jamii ili kukabiliana na changamoto za kiutamaduni, unyanyapa, kutengwa ambavyo ni vizuizi katika utoaji wa taarifa na huduma kwa wahanga wa ukatili katika jamii. Vitendo hivi vinachangia kukuza utamaduni wa ukimya na kukubalika kwa ukatili wa kijinsia katika jamii.

Wasaidizi wa kisheria wana mchango mkubwa katika kusaidia wahanga wa ukatili ndani ya jamii.

Kwa kutambua umuhimu wa wasaidizi wa kisheria, shirika la maendeleo la watu wa Ujuerumani (GIZ) kupitia mradi wa upatikanaji haki kwa wanawake na watoto (SAFE) kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria, umeandaa mwongozo huu rahisi wa kisheria unaoangazia vifungu vya kisheria kuhusu ukatili dhidi ya wanawake na watoto kwa lugha rahisi, inayoeleweka, na kwa kutumia mifano. Mwongozo unalenga kuwa nyenzo rejea kwa wasaidizi wa kisheria katika kutoa huduma za msaada wa sheria hususani kwa manusura wa ukatili ili kufikia haki. Pia

unaweza kutumika na jamii ili kujielimisha kuhusu haki zao na kuchukua hatua pale zinapovunjwa .

Majukumu ya wasaidizi wa kisheria

Wasaidizi wa kisheria wanatarajiwa kuzingatia kanuni za maadili zifuatazo:

- Uwezo wa kitaalamu
- Bidii na umakini katika kazi
- Kutunza siri za wateja
- Kuepuka mgongano wa kimaslahi
- Kufuata uaminifu na uadilifu wa kitaalamu
- Kufuata miongozo ya kisheria za watoa huduma za msaada wa kisheria
- Kufuata utawala wa sheria

Wasaidizi wa kisheria wana wajibika kwa watu wanaowapatia msaada, kwa msajili wa msaada wa kisheria na kwa mahakama. Ikiwa msaidizi wa kisheria atakiuka kanuni za maadili, anaweza kuchukuliwa hatua za kisheria.

Wasaidizi wa kisheria wana wajibika kwa watu wanaowapatia msaada, kwa msajili wa msaada wa kisheria na kwa mahakama.

Katika kutoa msaada wa kisheria kwa waathirika wa ukatili dhidi ya wanawake na watoto, kulingana na majukumu yaliyowekwa kwenye Sheria ya Msaada wa Kisheria, wasaidizi wa kisheria wanapaswa:

i. Kuwashauri manusura kuhusu mchakato wa jinai na jinsi mfumo wa haki unavyofanya kazi.

ii. Kumsindikiza manusura hadi kituo cha polisi ilikutoa taarifa rasmi ya tukio, watu walioshiriki na mahali lilipotokea.

Angalizo: *Ni muhimu taarifa zote zifikishwe polisi kwa kuwa malalamiko hayo ndiyo msingi wa uandaaji wa hati ya mashtaka ya kosa hilo la jinai.*

iii. Kumsindikiza manusura hadi vituo vya afya kwa ajili ya uchunguzi wa kitabibu na matibabu. Pamoja na uchukuaji wa ushahidi wa kimahakama.

iv. Kuwaunganisha manusura na watoa huduma wengine kulingana na mahitaji kama vile maafisa ustawi wa jamii kwa ajili ya ushauri na msaada wa kibinadamu.

v. Kusaidia kufuatilia mwenendo wa kesi kwa kushirikiana na polisi na waendesha mashtaka kuhakikisha ushahidi wote unakusanywa.

vi. Kushirikiana na wasaidizi wengine wa kisheria na mawakili wanaosaidia kwenye kesi husika pale inapohitajika.

vii. Kumsindikiza manusura mahakamani iwapo kesi imefikishwa mahakamani na kama kuna uhitaji huo.

viii. Kuwezesha mawasiliano na ushirikiano kati ya manusura/mteja na familia yake wakati wa uchunguzi na mwenendo wa kesi mahakamani.

02

UKATILI DHIDI YA WANAWAKE NA WATOTO

UFAFANUZI WA DHANA

Ukatili dhidi ya wanawake na watoto

Ni moja ya ukiukwaji wa haki za binadamu ulioenea zaidi duniani. Ukatili huu unajumuisha aina mbalimbali za unyanyasaji ikiwa ni pamoja na ukatili wa kimwili, kingono, kihisia na hata wa kiuchumi, na mara nyingi huathiri zaidi wanawake na watoto.

Ukatili dhidi ya wanawake na Watoto ni sehemu ya ukatili wa kijinsia, ambao husababishwa na mizizi ya mfumo dume na ubaguzi wa kijinsia. Ingawa wanaume pia wanaweza kuwa waathirika, lakini wanawake na wasichana huathirika kwa kiwango kikubwa zaidi kutokana na miundo ya kijamii inayothamini wanaume zaidi, ikisababisha wanawake kuwa tegemezi kiuchumi na kukosa ulinzi wa kisheria. Aina hizi za ukatili zinachochewa na utegemezi wa kiuchumi, mila potofu, udhaifu wa mifumo ya sheria, na athari za migogoro ya kijamii.

Ingawa wanaume pia wanaweza kuwa waathirika, lakini wanawake na wasichana huathirika kwa kiwango kikubwa zaidi kutokana na miundo ya kijamii inayothamini wanaume zaidi, ikisababisha wanawake kuwa tegemezi kiuchumi na kukosa ulinzi wa kisheria.

Kupambana na ukatili huu kunahitaji mbinu shirikishi na ya kina inayojumuisha:

- Mabadiliko ya kisheria
- Elimu kwa jamii
- Mifumo salama ya msaada kwa waathirika
- Ushiriki wa jamii kwa ujumla

Ni muhimu kuachana na mila na mitazamo potofu ya mfumo dume pamoja na kuhimiza heshima ya pande zote kwa lengo la kujenga jamii yenye haki na usalama kwa kila mtu.

Aina za Ukatili dhidi ya wanawake na watoto

Kuna aina sita kuu za ukatili dhidi ya wanawake na watoto kulingana na vitendo vinavyofanyika na madhara wanayopata manusura. Mwongozo huu unaangazia aina tano zinazojumuisha makosa ya jinai kama inavyoonyeshwa hapo chini. **Ukatili wa kiuchumi** haujajumuishwa kwenye mwongozo huu kwa kuwa matendo hayo hushughulikiwa katika taratibu za kimadai.

Ukatili wa Kimwili

Matendo ya makusudi yanayolenga kusababisha madhara ya kimwili kwa kutumia mwili wa mtu au vitu.

Mfano: Kupiga kofi, kupiga teke, kukaba, kupiga ngumi, kusukuma, kuvuta, kushika kwa nguvu, n.k.

Ukatili wa kingono

Kitendo chochote cha kingono, matamshi au vitendo vya kingono vinavyofanywa bila ridhaa ya mtu, au tabia nyingine yoyote inayoelekezwa kwa mtu kwa misingi ya jinsia au hali ya kingono.

Mfano: Kubakwa, kushikwa isivyofaa, kunyanyaswa kingono, kupapaswa bila idhini, kuombwa penzi kwa nguvu, n.k.

Ukatili wa kihisia

Kitendo au kuacha kufanya jambo na kusababisha madhara ya hisia kwa mtu.

Mfano: Matusi, dharau, kejeli, vitisho, kumlazimisha mtu kushiriki katika vitendo vya udhalilishaji, kumtenga na familia au marafiki, au kumzuia kuwasiliana na wengine au kutoka nje.

Ukatili unaowezeshwa na Teknolojia

Aina yoyote ya ukatili inayofanywa kwa kutumia teknolojia ya kidijitali au mtandao kama vile simu, kompyuta, na vifaa vingine vya mtandao.

Mfano: Unyanyasaji mtandaoni, uonevu wa mtandao, kufuatilia watu mtandaoni, vitisho mtandaoni, n.k.

Sababu za Ukatili dhidi ya wanawake na watoto

Mila na desturi za jamii

Zilizojengwa katika misingi ya mfumo dume, imani za kitamaduni, mitazamo na maoni yanayoweka wanaume juu na kuwanyima wanawake nafasi ya kushiriki katika maamuzi, umiliki wa mali, na udhibiti wa rasilimali.

Wanawake na watoto huonekana kuwa chini au mali ya mwanaume hali inayochochea manyanyaso na ukatili.

Mifumo ya kiuchumi ya kijamii

Mfano: fursa finyu za kiuchumi na ajira kwa wanawake, na ukosefu wa udhibiti wa rasilimali za kiuchumi. Hali hii husababisha wanawake kupata kipato kidogo na kuwa tegemezi.

Umaskini pia huongeza hatari kwa watoto wa mitaani na wasichana wadogo kulazimika kufanya kazi hatarishi au kuolewa mapema.

Malezi ya kijamii na familia

Kuishi kwenye mazingira yenye ukatili, unyanyasaji au kutelekezwa, kwenye kusababisha kukubalika kwa ukatili kama jambo la kawaida, matumizi mabaya ya dawa za kulevya au pombe, hali ambayo husababisha kushindwa kufanya maamuzi sahihi, hasira, na kushindwa kujisimamia.

Mfumo wa kisheria na kitaasisi

Udhaifu na changamoto katika kulinda manusura wa ukatili ipasavyo na kuwawajibisha wahalifu wa ukatili wa kijinsia. Sheria za kibaguzi, urasimu wa kitaasisi na rushwa husababisha uonevu kwa manusura na upendeleo kwa wahalifu wa ukatili.

Madhara ya Ukatili dhidi ya wanawake na watoto

KIMWILI

Maumivu, Majeraha, Kupoteza uwezo wa kutumia viungo vya mwili kwa muda au kabisa, Ulemavu, Kifo

KIJINSIA

Kuambukizwa magonjwa ya zinaa, Kuambukizwa virusi vya UKIMWI, Kukatwa au kuharibiwa sehemu za siri, Mimba zisizotarajiwa, Utoaji mimba/kuua watoto wachanga, Mimba kuharibika kwa wanawake wajawazito

KIJINSIA

Hofu/vitisho/kuto kujiamini; Kujihisi kutokuwa na thamani; aibu; Kukosa hamasa, kujitenga; Magonjwa ya akili – msongo wa mawazo/ sonona; Tabia hatarishi – matumizi ya pombe au dawa za kulevya; Kukosa uwezo wa kuchukua hatua au uthubutu

KIUCHUMI

Gharama za kifedha kulipia huduma za afya na michakato wa kisheria; Utendaji duni wa kazi; Kutohudhuria kazini au shughuli za kiuchumi kwa sababu ya kupata matibabu au kushughulikia kesi za kisheria; Kupoteza fursa za kupandishwa cheo au kupata kazi kutokana na kukosa ari, kujiamini na kujiona usio na thamani; Utegemezi; Umaskini

03

MUHTASARI WA SHERIA MUHIMU NA MIFANO

MUHTASARI WA SHERIA MUHIMU NA MIFANO

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 (kama ilivyofanyiwa marekebisho mara kwa mara)

Hii ni sheria mama inayotoa haki, uhuru na wajibu wa watu na taasisi.

Sheria zote pamoja na utekelezaji wake zinapaswa kuzingatia Katiba, inavyotoa haki za msingi ambazo kila mtu anapaswa kufurahia, ikiwa ni pamoja na ulinzi dhidi ya ukatili kwa wanawake na watoto, yaani usawa wa kila mtu mbele ya sheria, kinga dhidi ya ubaguzi, haki ya kufurahia haki za msingi, na ulinzi chini ya sheria.

Sheria za Msingi

Hizi ni sheria mahususi zinazoshughulikia aina mbalimbali za vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto kama zilivyo ainishwa hapa chini:

i. **Sheria ya Kanuni ya Adhabu – Sura ya 16, Toleo la Mwaka 2022** Hii ni sheria kuu inayobainisha makosa ya jinai nchini, ikiwa ni pamoja na ukatili wa kimwili, kingono na kihisia. Maelezo zaidi yanapatikana katika vifungu mahususi vya sheria hii kama ifiuatavyo.

Na.	Makosa	Mifano
1	Ukatili wa kimwili / kushambulia mtu kimwili au kwa kutumia vitu/ chombo. **Kifungu cha 240, 241 na 225**	• Kumpiga kofi, kumkanyaga, kumbana, kumpiga ngumi, kumsukuma/kumvuta kwa nguvu. • Kumpiga na kitu vifaa vya nyumbani, viboko, mikanda, ubapa wa panga n.k. • Kumvunja mkono au mguu, kukata au kumng'oa masikio, mikono n.k.

Na.	Makosa	Mifano
2	Kutoa kwa kukusudia au kuwezesha mtu kupewa kitu hatari kwa afya au maisha yake. **Kifungu cha 227**	• Kumpa mtu kwa makusudi chakula au kinywaji chenye sumu au miti shamba kwa nia ya kumdhuru. • Kumpa mtu kemikali hatari, dawa haramu, dawa ya kuondoa madoa, sumu za kuua wadudu au kumpa usingizi mzito kwa nia ya kumuumiza
3	Kusababisha kifo kwa kukusudia au kutokukusudia **Kifungu cha 195, 196 na 197**	• Mume kumpiga mke kwa panga kichwani na kumsababishia kifo. • Mke kuchoma nyumba na mume akiwa ndani kwa lengo la kumuua • Mtu kumsukuma mwingine kwa hasira hadi kuanguka na kuvunjika kichwa, shingo na kufa. • Kumshawishi mtu aende sehemu ambapo unajua atadhuriwa/kuuwawa
4	Jaribio la kuua **Kifungu cha 211**	• Mtu kujaribu kumuua mwingine au kuchukua hatua zinazoelekea kuhatarisha maisha yake. • Kupiga risasi kwa lengo la kuua lakini risasi ikakosea njia au ikasababisha majeraha tu. • Kuweka sumu kwenye chakula au kinywaji kwa lengo la kumuua lakini mtu akafikishwa hospitali mapema na kupona. • Kuchoma nyumba huku ukijua kuna mtu ndani, kwa lengo la kumuua lakini mtu akaokolewa.
	Ukatili wa Kingono – Vitendo au tabia zinavyofanywa bila ridhaa ya mhusika i.e • **Ubakaji kifungu cha 130(2) na 131**	• Mwanaume kujamiina na msichana bila ridhaa yake. • Kwa ridhaa yake endapo ridhaa hiyo imepatikana kwa kutumia nguvu, vitisho au hofu. • Kama msichana hayuko na akili timamu au amelewa. • Ridhaa imepatikana kwa kwa kutumia udanganyifu au maelezo ya uongo. • Kwa ridhaa au bila ridhaa yake endapo msichana huyo ana umri wa chini ya miaka 18. • Mwanaume kushiriki tendo la ndoa na mwanamke mwenye matatizo ya akili au aliyelewa au kuchanganyikiwa. • Kundi la wanaume kushiriki tendo la ndoa na mwanamke au msichana bila ridhaa yake.

Na.	Makosa	Mifano
4	• Unyonyaji wa Kijinsia **Kifungu cha 130(3)**	• Kulazimisha mtu kufanya ngono kwa ajili ya kupata mahitaji ya msingi kama chakula, hifadhi au usalama. • Mganga wa kienyeji kutumia nafasi yake kudai kufanya ngono kwa madhumuni ya tiba. • Kiongozi wa dini kutumia nafasi yake kufanya ngono na msichana au mwanamke.
	• Unyonyaji wa Kijinsia kwa Watoto **Kifungu cha 138B (1)**	• Watoto kuuzwa kwenye mitandao ya ukahaba na kulazimishwa kujiuza.
	• Kujamiana na ndugu **Kifungu cha 158**	• Kufanya mapenzi na ndugu wa damu kama baba, kaka, binamu au babu.
	• Kujamiiana kinyume na maumbile **Kifungu cha 154**	Mtu yeyote ambaye- • anamuingilia mtu yeyote kinyume cha maumbile au, • anamuingilia mnyama kimwili au • anamruhusu mwanaume kumuingilia yeye mwanaume au mwanamke kinyume na maumbile,
	• Ukeketaji **Kifungu cha 169A (1)**	• Mtu kukata, kuondoa, kuongeza urefu au kuweka vitu kwenye sehemu ya siri ya mtoto wa kike wa umri chini ya miaka 18.
	• Kutorosha **Kifungu cha 133**	• Mwanaume kumchukua msichana kutoka nyumbani kwao bila ridhaa yake na kumlazimisha kuolewa naye. • Mwanamke kufungiwa ndani na mwanaume iliakubali kufanya naye mapenzi.
	• Lugha chafu, mzozo na kutishia kutumia nguvu **Kifungu cha 89(1)**	• Mume au mke kumwita mwenza wake "mpumbavu", "bure", "mbaya" au "mbwa". • Mzazi kumwambia mtoto wake wa kike kuwa, "Ukifeli mtihani, atamkana." • Mume kumwambia mke wake kwamba atamuua ikiwa atajaribu kumuacha.

ii. Sheria ya Ndoa - Sura ya 29 Toleo la mwaka 2019

Na	Makosa	Mifano
1	Ndoa ya kulazimishwa – **Kifungu cha 38(1)**	• Mtu kulazimishwa kuolewa au kuoa bila ridhaa yake. • Familia kumwozesha mtoto wa kike ili kupata hela ya kulipa deni. • Familia kumwozesha binti kwa sababu amefeli shule. • Mwanaume kulazimishwa kumuoa msichana wa kabila lake. • Mwanaume kulazimishwa kumuoa msichana kwa sababu amempa mimba.
2	Kumpiga mwenza – **Kifungu 66**	• Kumpiga mwenza na kiboko au mkanda
3	Urithi wa mjane – **Kifungu cha 68(b)**	• Mjane kulazimishwa au kutarajiwa kuolewa na ndugu wa kiume wa marehemu mume wake.
4	Unyanyasaji wa mtoto – **Kifungu cha 13**	• Kusababisha madhara ya kimwili, kimaadili au kihisia, kama vile kumpiga, kumtukana, kumbaguwa, kumtelekeza, unyanyasaji wa kingono na ajira za kinyonyaji. • Mtoto kupigwa mara kwa mara kwa mkanda/ fimbo kwa makosa madogo hadi kuonekana na michubuko. • Mtoto kuambiwa mara kwa mara na wazazi wake kuwa hana maana na hatofanikiwa maishani. • Mtoto wa kike kubakwa na rafiki wa karibu wa familia na kutishiwa asiseme. • Mtoto mchanga kuachwa kwenye eneo la wazi na mzazi aliyeshindwa kumlea.

iii. Sheria ya Mtoto – Sura ya 13 Toleo la Mwaka 2019

Na	Makosa	Mifano
1	Unyanyasaji wa mtoto – **Kifungu cha 13**	• Kusababisha madhara ya kimwili, kimaadili au kihisia, kama vile kumpiga, kumtukana, kumbaguwa, kumtelekeza, unyanyasaji wa kingono na ajira za kinyonyaji. • Mtoto kupigwa mara kwa mara kwa mkanda/ fimbo kwa makosa madogo hadi kuonekana na michubuko.

Na	Makosa	Mifano
		• Mtoto kuambiwa mara kwa mara na wazazi wake kuwa hana maana na hatofanikiwa maishani. • Mtoto wa kike kubakwa na rafiki wa karibu wa familia na kutishiwa asiseme. • Mtoto mchanga kuachwa kwenye eneo la wazi na mzazi aliyeshindwa kumlea.

iv. Sheria ya Makosa ya Mtandao – Sura ya 50 Toleo la Mwaka 2022

Na	Makosa	Mifano
1	Unyanyasaji kwa kutumia njia ya kidigitali/mtandao: • Ponografia ya watoto – **Kifungu cha 13**	• Kuchapisha au kusambaza picha/video za ngono za watoto kwa kutumia mfumo wa kompyuta.
	• Ponografia – **Kifungu cha 14 cha sheria**	• Kusambaza picha au video za ngono kwa njia ya mtandao
	• Kuchapisha taarifa za uongo – **Kifungu cha 16**	• Kuchapisha taarifa za uongo mtandaoni kwa lengo la kumdhalilisha, kumtusi, kumshushia heshima au kumtisha mtu.
	• Ujumbe usiotakiwa – **Kifungu cha 20**	• Kutuma ujumbe ambao mtu hakuruhusu kutumiwa kama taarifa za waganga wa kienyeji, freemasoni, matusi au vitisho mara kwa mara.
	• Uonevu wa mtandaoni – **Kifungu cha 23**	• Kutuma ujumbe wa matusi, vitisho, taarifa za kumshushia hadhi au heshima au zenye kumfanya mtu ajisikie vibaya kwa kutumia mitandao ya kijamii na kumfuatilia mtu. • Kutishia kusambaza picha za faragha za mtu bila ridhaa yake. • Kuchapisha taarifa binafsi kama anuani ya nyumbani au namba ya simu ili mtu apata madhara. • Kujifanya mtu mwingine mtandaoni kwa lengo la kudanganya au kujinufaisha.

v. Sheria ya Elimu ya Taifa – Sura ya 353 Toleo la Mwaka 2022

Na	Makosa	Mifano
1	Marufuku kuoa au kumpa mimba mwanafunzi – **Kifungu cha 60A (1&2)**	• Kufunga ndoa au kumuweka unyumba na mvulana au msichana wa shule ya msingi au sekondari. • Kumshawishi au kumlazimisha mwanafunzi wa shule kuolewa. • Mtu kumpa mimba msichana wa shule ya msingi au sekondari

vi. Sheria ya Ukimwi (Kinga na Udhibiti), Na. 28 ya Mwaka 2008

Na	Makosa	Mifano
1	Unyanyapaa na ubaguzi – **Kifungu cha 31**	• Kumdhalilisha mtu kwa sababu anaishi au anahisiwa kuwa na VVU. • Kubeza au kumkataa mtu, kumletea aibu au kumfanya ajihisi duni kwa sababu ya VVU.
2	Maambukizi ya Makusudi **Kifungu 47**	• Mtu kumwambukiza mwingine VVU makusudi. • Mume au mke kumwambukiza mwenzake VVU kwa makusudi mfano kukataa kutumia kinga ukiwa unajua una maambukizi . – Kutofahamisha mwenza kuhusu hali yake ya VVU na kumwambukiza kimya kimya.

vii. Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Marekebisho)ya Mwaka 2024

Na	Makosa	Mifano
1	Kuomba au kulazimisha huduma za kingono – **Kifungu ca 25**	• Mtu mwenye mamlaka kuomba au kulazimisha mahusiano ya kingono au kufanya ngono ili kutoa kazi, kupandisha cheo au kutoa haki fulani. • Bosi au mwajiri kuomba ngono ili kufanikisha mkataba wa ajira, au mwalimu kuomba ngono ili kumpa mwanafunzi alama anayostahili.

04

HUDUMA ZA RUFAA KWA WAATHIRIKA WA UKATILI DHIDI YA WANAWAKE NA WATOTO

HUDUMA ZA RUFAA KWA WAATHIRIKA WA UKATILI DHIDI YA WANAWAKE NA WATOTO

Wakati wa utoaji wa msaada wa kisheria kwa manusura, wasaidizi wa kisheria wanapaswa:

- Kusikiliza kwa makini maelezo ya manusura,
- Kuelewa mahitaji yao,
- Kuwapatia taarifa sahihi kuhusu sheria na hatua za kuchukua.

Kuwawezesha manusura kufanya maamuzi yenye ufahamu na kutoa ridhaa yao kabla ya kuwaunganishwa na watoa huduma mbalimbali

Kuwawezesha manusura kufanya maamuzi yenye ufahamu na kutoa ridhaa yao kabla ya kuwaunganisha na watoa huduma mbalimbali za msaada wa kisheria, kiafya, kisaikolojia, kijamii na kibinadamu.

Hatua za kuchukua na huduma zinazotolewa kwa manusura wa ukatili kulingana na mahitaji yao:

MANUSURA/JAMII

- Tafuta eneo salama na mweleze mtu unayemwamini
- Toa taarifa polisi na kupata fomu ya polisi PF3 (ni bure)
- Piga simu ya dharura kwa polisi – namba 122
- Ripoti katika kituo cha afya
- Kwa manusura: usijisafishe, kuoga au kubadilisha nguo kabla ya ushahidi kuchukuliwa
- Manusura wa ukatili wa kingono: usikojoe au kutumia choo hadi sampuli zichukuliwe hospitalini

POLISI

- Manusura kuripoti na kutoa maelezo kamili kituoni; kusoma au kusomewa na mtu unayemuamini maelezo yao kabla ya kusaini.
- Baada ya kutoa taarifa, nenda kwenye kituo cha afya ndani ya masaa 72.
- Toa vielelezo vyovyote kama nguo kwa polisi ili kufungua kesi.

KITUO CHA AFYA

- Manusura watoe ridhaa yao kwa uchunguzi wa mwili, matibabu, na uchukuaji wa sampuli.
- Tiba na uchunguzi wa kiafya kwa manusura vifanyike ndani ya masaa 72.
- Kama manusura walianza katika kituo cha afya, watibiwe kwanza kisha waripoti polisi.
- Wapate ushauri wa kiafya na kisaikolojia.

USTAWI WA JAMII

- Manusura wanaweza kutoa malalamiko kuhusu migogoro ya ndoa na ukatili wa kijinsia.
- Kuomba hifadhi salama kama kuna hofu ya usalama wa maisha.
- Kupata huduma za usuluhishi, mazungumzo na maridhiano.
- Ufuatiliaji wa makubaliano yaliyofikiwa .
- Endapo kuna ukiukwaji au ukatili mkubwa, au kutokutekelezwa kwa makubaliano ya awali manusura kuelekezwa kwenda polisi au mahakamani.

WASAIDIZI WA KISHERIA

- Kuwapa taarifa manusura kuhusu mchakato wa kisheria ili wafanye maamuzi wakiwa na uelewa.
- Kusaidia kupunguza hatari na kulinda usalama wa manusura.
- Kuhakikisha taratibu za jinai zinamwezesha manusura kupata haki – kuwapa taarifa, kuwasiliana na polisi na waendesha mashtaka.
- Kurejesha na kuimarisha hali ya kujidhibiti na kujiheshimu kwa manusura kupitia ushauri wa kisheria na kisaikolojia kwa manusura na familia zao.

05

HITIMISHO

HITIMISHO

Mwongozo huu umeandaliwa kwa lugha rahisi ili kusaidia kukuza uelewa wa aina mbalimbali za makosa dhidi ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto na sheria.

Mwongozo huu umeandaliwa kwa lugha rahisi na nyepesi ili kusaidia kukuza uelewa wa aina mbalimbali wa makosa dhidi ya ukatili wa wanawake na watoto na sheria. Ni mategemeo kuwa mwongozo huu utawasaidia wasaidizi wa sheria na watoa huduma za msaada wa kisheria, kuelewa juu ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto, matukio ya ukatili pamoja na sheria zinazoyasimamia ili kuwasaidia manusura kwa ufanisi wakati wa utoaji wa ushauri na msaada wa sheria. Kwa changamoto za kisheria zilizo juu ya wigo wa mwongozo huu, inashauriwa kurejea kwenye sheria rasmi au kutafuta ushauri wa kitaalamu zaidi na huduma kutoka kwa wanasheria na mawakili.